BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani,
Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutanguliza shukurani zangu kwa Mwenyezi Mungu aliyetuumba na kutujaalia uhai na uzima wake uliotuwezesha kupata fursa hii adhimu na muhimu ya kukutana katika Mkutano huu wa Kumi na Tano kwa lengo la kuwatumikia wananchi pamoja na kutekeleza jukumu letu muhimu lililoelezwa katika kifungu cha 88 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kuhusiana na kazi moja kuu ya Baraza la Wawakilishi ya kupitisha Bajeti ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu inamshukuru na kumpongeza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Ndugu Othman Abass Ali pamoja na Watendaji wake kwa majibu na ufafanuzi waliokuwa wakiutoa wakati wa majadiliano ya kupitia Fungu la Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Aidha, kwa namna ya pekee tunampongeza Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Mwalimu Haroun Ali Suleiman kwa kuwasilisha vyema Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi hii muhimu kwa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na Kamati ya PAC kuwa na jukumu la kuchunguza na kujadili Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali lakini pia ina jukumu jengine la kujadili bajeti ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama inavyoelekezwa na Kanuni ya 107 ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la Mwaka 2020).

**Mheshimiwa Spika,** kabla ya kutoa Maoni na Mapendekezo ya Kamati yetu,

naomba kwanza kuwatambua Waheshimiwa Wajumbe pamoja na Makatibu wetu ambao walishiriki ipasavyo kujadili utekelezaji wa bajeti pamoja na mapendekezo ya bajeti yaliyowasilishwa mbele ya Kamati kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Juma Ali Khatib | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Bakar Hamad Bakar | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Jamal Kassim Ali | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Miraj Khamis Mussa | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Shadya Mohammed Suleiman | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Kombo Mwinyi Shehe | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Mohamed Ahmada Salum | Mjumbe |
| 9. | Ndg. Maryam Ali Haji | Katibu wa Kamati |
| 10. | Ndg. Said Khamis Ramadhan | Katibu wa Kamati |
| 11. | Ndg. Fatma Omar Ali | Katibu wa Kamati |
| 12. | Ndg. Adam Maulid Simai | Katibu wa Kamati |

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhishwa na utekelezaji wa Bajeti ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2023/2024 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi hiyo kwa mwaka 2024/2025 kama yalivyoainishwa katika Fungu E04 la Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, Kamati ya PAC imetoa ushauri mahsusi na ushauri wa jumla katika maeneo yanayohusika na makadirio ya bajeti hiyo ili Bajeti ya Afisi hii iweze kutekelezeka ipasavyo na kuleta tija inayokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa muda mrefu wakati Kamati ya PAC ikiwasilisha hotuba zake kuhusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hukumbushia kitendo cha upangaji wa Makusanyo ya Mapato ya Afisi hiyo unaofanywa na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango bila ya kuzingatia uwezo halisi wa chanzo cha Taasisi hiyo katika ukusanyaji mapato yaliyopangwa, suala hilo hutoa

taswira mbaya katika ufanisi na utendaji wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** historia inaonesha wazi uwezo halisi wa ukusanyaji wa mapato ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali umekuwa haufikii lengo la ukusanyaji wa mapato lililopangwa kwa kila mwaka wa bajeti. Hali hiyo hujitokeza kutokana na kuwepo idadi maalum ya Taasisi ambazo hutakiwa kufanya makusanyo ya malipo ya ada ya ukaguzi wa hesabu inayopangwa na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango.

**Mheshimiwa Spika,** mtiririko wa upangaji wa Bajeti ya makusanyo hauoneshi mlingano wa makusanyo halisi. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilipangiwa kukusanya jumla ya Shilingi Milioni 250,000,000 wakati kiuhalisia ilipata jumla ya Shilingi Milioni 60,744,000 sawa na asilimia 38 wakati kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Afisi hiyo ilipangiwa kukusanya jumla ya Shilingi Milioni 283,012,000 ambapo hadi kufikia mwezi wa Machi, 2023 ilifanikiwa kukusanya jumla ya Shilingi Milioni 55,053,000 sawa na asilimia 24.5 ya makadirio. Aidha, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Afisi hiyo ilipangiwa kukusanya jumla ya Shilingi Milioni 325,000,000 ambapo hadi kufikia mwezi wa Machi, 2024 ilifanikiwa kukusanya jumla ya Shilingi Milioni 73,000,000 sawa na asilimia 22.4 ya makadirio.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na mtiririko huo wa makusanyo ya Afisi hii ambao kwa muda wa miaka mitatu haukuweza kufikia hata asilimia 40 ya makusanyo yao, inaonesha wazi kwamba uwezo halisi wa makusanyo yake unatakiwa ufanywe baada ya kufanyika kwa utafiti wa kina kuhusiana na makusanyo yao kwa kulinganisha na chanzo chake kimoja cha mapato cha ada za ukaguzi.

**Mheshmiwa Spika,** katika kulitathmini hilo, Kamati yetu ilitaka kujua vigezo vinavyotumika katika kuandaa makadirio ya mapato kwa Afisi hiyo na kuelezwa kwamba Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ndio inayohusika na upangaji huo ambapo hufanyika bila ya kufanya utafiti wa vyanzo vya mapato vya Afisi ya Mdhibiti pamoja na kutowashirikisha ipasavyo Watendaji wa Afisi hiyo wakati wa ukadiriaji. Kinachofanyika ni kupanga makadirio kwa kuangalia bajeti iliyopangwa katika mwaka uliopita. Lakushangaza zaidi, suala hili limeshasemwa san a hapa Barazani kwamba

Afisi ya Rais, Fedha na Mipango wanapopanga makadirio ya mapato wasiangalie taswira ya Afisi husika isipokuwa wazingatie uwezo halisi wa vyanzo vya makusanyo.

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kupitia Mapato ya Makadirio ya Bajeti ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kamati ya PAC imebaini kwamba lengo la ukusanyaji mapato halikuweza kufikiwa kutokana na kutolipwa kwa madeni ya muda mrefu ya malipo ya ada ya ukaguzi ambayo Afisi ya Mdhibiti imeelekezwa kutoza kwa baadhi ya Taasisi za Serikali zinazopatiwa huduma ya ukaguzi. Hadi Kamati inawasilisha hotuba yake mbele ya Baraza lako, jumla ya Shilingi Milioni 134,600,000.00 zinadaiwa kwa Taasisi za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa Taasisi za Serikali zinazodaiwa ada ya ukaguzi na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni pamoja na Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC), Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA), Shirika la Nyumba (ZHC), Kampuini ya Uvuvi (ZAFICO), Mamlaka ya Uwekezaji (ZIPA), Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA), Wakala wa Uchapaji Zanzibar (ZAGPA), Kampuni ya Mafuta (ZPDC) na Kampuni ya Ujenzi ambapo kila Taasisi inadaiwa shilingi milioni 8,800,000. Aidha, Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC), Shirika la Magazeti, Mamlaka ya Mafunzo ya Amali, Afisi ya Mthamini Mkuu na Bodi ya Wasanifu Majengo ambao kila Taasisi inadaiwa shilingi milioni 7,000,000.

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi zote hizo ukizitathmini utagundua kuwa ni Taasisi zenye uwezo kifedha ambazo Kamati yangu haikutegemea kuonekana kushindwa kulipa madeni yao ya ada za ukaguzi kwa Taasisi husika.

**Mheshimiwa Spika,** iwapo madeni hayo yangelipwa kwa wakati, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ingeweza kufikia lengo lake la makusanyo yaliyokadiriwa kwa kufikia zaidi ya asilimia 80.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu pia imegundua kwamba Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali haipo huru ipasavyo katika kujipangia Taasisi za kukusanya malipo ya ada ya ukaguzi pamoja na kiasi cha malipo wanayotakiwa kutoza kwa Taasisi hizo. Badala yake, Afisi hiyo

hupokea maelekezo kutoka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kupitia barua rasmi ambayo hutolewa katika kila mwaka wa fedha. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeelekezwa kutoza malipo ya ada ya ukaguzi kwa Mashirika, Taasisi za Kati, Wakala na Taasisi ndogo 25 za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hata hivyo, baadhi ya Taasisi hizo hawakuweza kufanya makusanyo kutokana na ama kuunganishwa na Taasisi nyengine au kwa maumbile yake kushindwa kujitegemea kifedha.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokuwa ikipitia Programu Ndogo ya SE040101 inayohusiana na Ukaguzi wa Fedha na Rasilimali za Umma ilibaini uwepo wa ongezeko la matumizi kutoka Shilingi Bilioni 2,373,721,000 hadi kufikia Shilingi Bilioni 2,940,643,012 ikiwa ni ongezeko la Shilingi Milioni 566,922,012 sawa na asilimia 123 ambapo baada ya Kamati kuhoji uhalali wa matumizi hayo ilielezwa kwamba ongezeko hilo limetokana na kufanyika kwa ajira mpya ambapo bajeti ya ajira hiyo haikuwemo katika makadirio ya awali ya Afisi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu inashauri kwamba ili Wajumbe wako waweze kupata fursa ya kupitia makadirio ya mapato na matumizi ya Afisi hii na kuishauri Serikali ipasavyo, ni busara kwa Watalaamu wetu wawe wanaandaa mchanganuo mzuri katika RIpoti ya utekelezaji wa bajeti ya Afisi ya Mdhibiti utakaoonesha kiuwazi sababu zilizopelekea ongezeko la matumizi yaliyojitokeza na kufanya fedha za Programu ndogo husika kuonekana kuwa nyingi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu imepatwa na mshangao ilipokuwa ikijadili Programu ndogo ya **SE040203** kwa kubaini kwamba Mfumo wa PBB unaotumiwa na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango katika kupanga makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Serikali hushindwa kufuta taarifa za kifedha za miaka mitatu iliyopita. Hili limebainika kwa kuhoji uwepo wa Idara ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti ambayo kwa mwaka huu wa fedha haikuingiziwa fedha kutokana na shughuli zake kuhamishiwa katika Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ya Wizara. Aidha, Kamati imegundua kuwepo kwa Wafanyakazi 9 na Wafanyakazi wengine 11 ambao walipatiwa mafunzo ya muda mrefu lakini kiuhalisia ni Wafanyakazi 11 tu ndio waliopatiwa mafunzo hayo.

**Mheshimiwa Spika**, hali hiyo imewafanya Wajumbe wako kuhoji kwamba Watendaji waliopatiwa mafunzo ni 11 au 20 na kujibiwa kwamba Wafanyakazi husika ni 11 kwa Unguja na Pemba ambapo Wafanyakazi 9 wanaoonekana ni wa mwaka jana lakini hawakuweza kuwaondoa kwa vile Mfumo unakuwa unaendelea kutambua taarifa za miaka mitatu iliyopita.

**Mheshimiwa Spika,** kuwepo kwa Mfumo usioweza kufuta taarifa za kipindi kilichopita kunapekelea uwepo wa mkanganyiko kwa wasomaji wa taarifa hizo za bajeti pamoja na kukosa uhalisia wa taarifa sahihi na halisi za kibajeti.

**Mheshimiwa Spika,** Hivyo, Kamati yangu inaishauri Serikali kulitafutia utatuzi wa haraka suala hili ili taarifa za bajeti kwa kila Programu ziendane sambamba na uhalisia wa kinachotekelezwa kwa Idara au Taasisi husika. Aidha, kufanya hivyo kutapunguza kuwepo kwa taarifa nyingi na bajeti.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako waijadili, waichangie na kuiunga mkono bajeti hii ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka wa fedha 2024/2025 na hatimae kumuwezesha Mdhibiti kwenda kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC), naunga mkono hoja hii kwa asilimia Mia Moja na naomba kuwasilisha.

…………………
Mhe. Juma Ali Khatib,
Mwenyekiti,

Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC),

**BARAZA LA WAWAKILISHI,**

**ZANZIBAR.**